# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## KIKAO CHA AROBAINI NA NANE

**14 JUNI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### KIKAO CHA AROBAINI NA NANE – TAREHE 14 JUNI, 2023

## I. DUA:

## II. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**618. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni faida gani ambayo Wafanyakazi wanapata kupitia uwekezaji wa fedha wanazokatwa na Vyama vya Wafanyakazi.

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**619. MHESHIMIWA SAMWEL XADAY HHAYUMA (HANANG'):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Mogitu – Dawar hadi Ziwa Chumvi ili kusafirisha Chumvi ghafi kwenda Kiwandani.

**620. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Ninde, Masokolo hadi Lupata katika Kata ya Kuzumbi.

**621. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga barabara za lami katika Mji wa Mombo.

**622. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha kumalizia ujenzi wa Vituo vya Afya vya Matwiga na Mafyeko Jimboni Lupa.

**623. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini hatma ya Barabara ya Zakhiem Mbagala Kuu inayoshindwa kujengwa kwa kuwa bomba la mafuta lipo chini ya barabara.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**624. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ipo tayari kuwapandisha Vyeo kwa mserereko kufikia Daraja wanalostahili Watumishi waliosubiri zaidi ya miaka 8 Kyerwa.

**625. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza siku za likizo kwa Wazazi wanaojifungua Watoto Njiti.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**626. MHESHIMIWA MWATUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha na kuwainua kiuchumi Wanawake wasiojiweza.

**WIZARA YA NISHATI:**

**627. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Ujenzi wa Kv 400 kutoka Iringa, Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga utaanza pamoja na kulipa Wananchi waliopitiwa na laini hiyo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**628. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani kusaidia Halmashauri zinazozunguka Mbuga/Hifadhi za Taifa kupitia *CSR* kutoka kwenye mapato ya utalii.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**629. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Nduguti kwa kuwa ujenzi wake umesimama kwa muda mrefu.

**630. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGIDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilayani Kishapu.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**631. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya njia nne kuanzia Tengeru utaendelea ikiwa ni mwendelezo wa Barabara ya Sakina - Holili.

**632. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya kutoka Kibada – Tundwi hadi Songani kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**633. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga Minara ya Simu maeneo yasiyo na mawasiliano hususan Kata za Ipwani, Miyombweni na Igava.

**WIZARA YA KILIMO:**

**634. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa bwawa katika Kijiji cha Ichemba.

**635. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kufanya utafiti ili kubaini mazao yanayoweza kustawi Mkoa wa Mtwara kama mbadala wa zao la korosho.

**WIZARA YA MAJI:**

**636. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini changamoto ya upatikanaji maji katika Mji wa Mlowo itatatuliwa.

**637. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini mradi wa maji Kata za Kaengesa na Kanda Sumbawanga Vijijini utakamilika.

**DODOMA** **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**14 JUNI, 2023** **KATIBU WA BUNGE**